

# KARIBU KWENYE MAKALA YA **KVTC H2 2024!**

## Wapendwa Wasomaji,

Tumehamasika kuwaletea makala ya sasa ya KVTC! Katika Makala hii tunaelezea habari za kusisimua kuhusu mambo mapya, za kufikirisha, na yaliyojiri katika kampuni, kuku habarisha na kukushirikisha. Utasoma kuhusu shughuli na miradi iliyotekelezwa kuanzia Juni 2024. Tunashukuru kuwa miongoni mwa wanajamii wetu. Tunatumaini unafurahia makala hii na tunarajia utakuwa nasi, kama ilivyokuwa kawaida jisikie huru kushirikishi mawazo yako na. Tunapenda kusikiliza mrejesho kutoka kwako.

Soma kwa furaha!

kvtc@kvtc.co.tz
www.kvtc.co.tz
P.o.Box 655 Mavimba,Ulanga, Morogoro
Tanzania



# Mfanyakazi mpya katika Familia ya KVTC



Sarah Mtelele
**Meneja Raslimali Watu na Mahusiano**

Sarah Mtelele alijiunga na KVTC kama Meneja Raslimali Watu na Mahusiano ya Kampuni Julai Mosi 2024. Majukumu yake ni pamoja kusimamia majukumu yote ya raslimali watu, mafunzo na uendelezaji, mahusiano kazini, mishahara na mahusiano ya kampuni na wadau wake wote wa nje.

Bi Sarah Mtelele ni mtaaluma aliyebobea katika maswala ya raslimali watu ana uzoefu zaidi ya miaka 14 katika kusimamia na kuendeleza vipaji katika sekta mbalimbali kama benki na fedha, Uzalishaji, usafirishaji na mpangilio (Logistics), biashara na rejareja. Sarah ana uwezo kujenga utamaduni wa mazingira shirikishi kazini, kuimarisha ushiriki wa mfanyakazi na kuleta ukuaji wa taasisi kupitia jitihada za ubunifu wa raslimali watu. Anafahamika kwa mkakati lakini mtaratibu katika usimamizi wa raslimali watu.

Kabla ya kujiunga na kampuni ya Mitiki bonde la Kilombero, Sarah alifanya kazi na kampuni Tanzu ya sekta binafsi (Private Sector Foundation) akiwa ni Mkuu wa idara utawala na raslimali watu. Amehitimu digrii ya pili katika fani ya usimamizi wa raslimali watu chuo kikuu cha Mzumbe na shahada ya Biashara katika masoko chuo kikuu cha Dar Es Salaam.
Sarah ni mfanyakazi muhimu sana katika ngazi ya uongozi na anaimudu vizuri bila shaka.

# Nini tumejifunza?

Katika muhula wa pili wa mwaka, KVTC inaendelea kuimarisha taaluma kwa wafanyakazi kwa kutoa mafunzo ya kitaalamu kwa kitengo cha misitu na uchakataji kuhakikisha kuna uendelevu wa mazao bora. Asilimia 90% ya mwaka wa fedha 2024 melees katika kuimarisha ujuzi wa kiufundi.



Wafanyakazi wa uvunaji katika Mafunzo ya moja kwa moja juu ya Mafunzo ya vitendo na mwenzeshaji Allan Ogram Royden kutoka CMO, South Africa.



Wasimamizi wa Kiwandani wakiwa wanapata mafunzo na mwenzeshaji Walter Mushi kutoka kwa Kituo cha Mafunzo ya Misitu na viwanda vya mbao (FWITC)

# Miaka 15 ya Uadilifu

KVTC inajivunia kuwa wafanyakazi wengi wenye kujitoa na makini waliofanya kazi kwenye kampuni kwa miaka zaidi ya 25. KVTC inatambua na kutoa zawadi kwa wafanyakazi wanao fanya kazi kwa kampuni zaidi ya miaka mitano. Mwaka huu tunasherekea wafanyakazi 15 kwenye vitengo tofauti vya shaughuli zetu.



Kutoka kushoto Kwenda kulia ni Thabit Utwa, Pius Mfanyakazi, Halima Kigona, Namikoa Zidadu, Yasin Saanane, Dennis Matimbi, Onesmo Lupembe and Beda Kangonga.

Wafanyakazi waadirifu wengine waliotimiza miaka 15 ni Amidu Karim, Selemani Mkumba, Thadei Masati Mussa Mtonyole, Khadija Bakari, and Ombeni Luoga.



# Dawati la Usalama na Afya

KVTC ni muumini wa utamaduni imara wa afya na usalama kazini situ inalinda wafanyakazi dhidi ya kuumia na magonjwa lakini vilevile inachangia mazingira mazuri ya kazi, kuongeza motisha na inaimarisha sifa ya kampuni. Afya na usalama ni kipaumbele cha juu. Tuna thamini khali nzuri ya wafanyakazi, ufanisi wa uzalishaji na mafanikio ya jumla.



Maelekezo ya mara kwa mara ya afya na usalama yanafanyika katika shughuli zote.

KVTC inatoa Mafunzo ya afya na usala-ma kwa wafanyakazi wake.





KVTC inaendesha shughuli za upimaji wa virusi vya ukimwi HIV na kansa kwa wafanyakazi wake kuhakikisha wafanyakazi wake wanajua khali zao za afya na wanachukua hatua za lazima ikiwa ni muhimu.

# Kuwafikia Wadau na Jamii

## Maonesha Nanenane

KVTC ilishiriki maonesho ya NaneNane 2024 yaliyofanyika Morogoro. Maonesho yaliwaleta washiriki na wageni kutoka Morogoro na mikoa Jirani. Ilikuwa ni fursa kwa KVTC kuonyesha bidhaa zake na kuelimisha wageni juu ya usimamizi wa mashamba ya mitiki na programu ya kusaidia wakulima wa nje ambayo KVTC imekuwa ikitekeleza kuanzia 2002

## Maazimisho ya Miaka 50 ya Mafunzo ya Misitu Tanzania

KVTC ilijiunga na Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA) katika kusherekea miaka 50 ya mafunzo ya Misitu Tanzania kuanzia Septemba 30 hadi Oktoba 4, 2024. SUA ni mbia wa KVTC katika elimu na tafiti. Taasisi zote mbili zimenufaika na shughuli nyingi za pamoja kwa miaka mingi. Sherehe ilijumuisha maonesho na jukwaa la majadiliano kuhusu maada mbalimbali zinazohusiana na mabadiliko ya elimu na mafunzo ya misitu  Tanzania na mabadiliko ya tabia nchi na athari zake.

Wafanyakazi wa KVTC walishiriki katika kongamano lililo husisha wanazuoni na wataalamu katika kilimo, utalii na wanyama pori kutoka sekta ya umma na binafsi. Washiriki walijadili mambo yanayohusu sekta yao na jinsi gani kupanga kwa mustakabali mzuri zaidi kwa wote hapo baaadaye.

KVTC ilionyesha bidhaa zake wakati wa tukio












KVTC

kvtc@kvtc-tz.com

www.kvtc.co.tz

P.o.Box 655 Mavimba,Ulanga, Morogoro Tanzania